



SAUTI ya Mtakatifu MARKO

Toleo la Pekee

Toleo kwa ajili ya Sala za Wakristu nyumbani

Familia iwe Kanisa la Msingi

Kuna wakati wa kupeleka familia kwa Kanisa, na kuna wakati, kama sasa, wa kuleta Kanisa ndani ya familia.

Twasema kwamba familia lake pia li hai. Maombi na huruma nyumbani watoto hupata mafunzo ya msingi ya kijiama na kikanisa pia: wanajifunza tabia, maombi, na zaidi ya hayo mifano ya maisha ya Kikristu. Tena, familia ni Kanisa la msingi kwa sababu Wakristu lazima waanze nyumbani kutimiza amri ya kupendana, kusaidiana, kusameheana, kuheshimiana. Na maombi pia: Tusali nyumbani!

Janga la Coronavirus (ama Covid-19), mwaka huu, limesababisha tofauti kubwa katika maisha ya kawaida. Hakuna shule, hakuna mikutano, hakuna ibada Kanisani. Wala hatuaweza kuwa pamoja katika ibada za Pasaka, wala katika Sherehe ya Mta-

katifu Marko, tarehe 25 Aprili. Katika nchi zingine, watu wengi wamekufa kwa sababu ya ugonjwa huu. Serikali ya Kenya imeamuru mapema tuanze kujilinda tuna-vyostahili. Kwa muda ambao hatujajua, hatutaweza kupatana kanisani. Hakuna Kanisa: je, hata imani imefungwa? Hata maombi hakuna? Hata bidii ya kusaidiana imesimamishwa? La, sivyo. Lazima wakati huu tujifunze kufanya familia iwe Kanisa!

Yesu yu hai: tumekumbuka ukweli huu siku hizi za Ufufuko. Pia Kanisa lazima liwe hai! Hata kama halionekani sana wakati huu. Kwa hivyo, Wakristu wenzangu, wakati huu tukumbuke sana mambo haya:

1) MAOMBI: katika familia, katika siri ya moyo, tuzidi kusali, kusikia Neno la Mungu, kulisha imani yetu ya Kikristu.

2) HURUMA: Kukaa mbali na watu kwa sababu ya ugonjwa, kusiwe kukaa mbali na mioyo yao, bali, kutufanye kuwa macho hata zaidi. Tuan-galie sana wenye shida, na tuwe tayari kusaidiana nao kwa njia yoyote.

3) HAKI YA AFYA: Ugonjwa huu unafanya tuwe tukilinda zaidi afya yetu na afya ya watu wengine. Tuwajali watu wote, tukitumia zile njia za kujilinda: kunawa, kufunika mdomo, kukaa mbali na watu wengine. Tutahepa hatari hiyo, tukijitolea sote pamoja.

Basi, na tupande mbegu ya imani katika familia zetu, vile tulivyoshughulikia sana mashamba yetu siku hizi za mvua! Na Mungu akubali kutuepushia hatari hii: aturudishie upesi ile furaha ya kuwa pamoja katika ibada ya Kanisa tunayohitaji sana, lakini mioyo yetu imkaribie yeye zaidi hata wakati huu.

Fr. Giacomo Basso - Baba Paroko

LAIKIPIA COUNTY EMERGENCY FUND

- Ni msaada wa chakula uliopangwa na Laikipia County kwa ajili ya wasiojiweza wakati huu wa janga la Coronavirus. Makanisa yanasaidiana na Serikali ya County.
- Wananchi wameombwa kuchangia na pesa au na chakula, pia kuwajulisha viongozi na wachungaji kuhusu wenye shida zaidi.
- Kwa eneo la Ol Moran, mwakilishi wa County na Makanisa ni Pst. Richard Mwangi, na Deliverance Church ya Ol Moran itakuwa mahali pa kuleta na kupeana msaada (yaani *Distribution Point*)

COVID-19 PREPAREDNESS

LAIKIPIA COUNTY EMERGENCY FUND

LISHA FAMILIA KOMESHA CORONA

DONATE TODAY

40,000+ HOUSEHOLDS NEED THIS AID

DROP FOOD DONATIONS HERE:

1. Wagonia Church - Nyakurui	11. Shalika Supermarket - Nyakurui	21. Deliverance Church - Muthurua
2. Quile Church - Nyakurui	12. St. Mark's Catholic Social Apostolate - Nyakurui/Karibia	22. PCCA Church - Muthurua
3. Janga Supermarket - Nyakurui	13. Janga Supermarket - Nyakurui	23. Janga Supermarket - Nyakurui
4. Mago Supermarket - Nyakurui	14. Mago Supermarket - Nyakurui	24. Direct Agribusiness - Nyakurui
5. Mt. Kenya Supermarket - Nyakurui	15. Mt. Kenya Supermarket - Nyakurui	25. Coast Road Supermarket - Nyakurui
6. Chief's Office - Nyakurui	16. Deliverance Church - Muthurua	26. Super Society Store - Nyakurui
7. St. Paul's Supermarket - Nyakurui	17. Catholic Mission - Nyakurui	27. Basha's Supermarket - Nyakurui
8. PCCA Church - Muthurua	18. Gospel Outreach - Nyakurui	28. Duka US Super Store - Nyakurui
9. SIDA - Mago Nyakurui	19. Mt. Kenya Catholic Church - Nyakurui	29. Mago Supermarket - Nyakurui
10. Olmorog Supermarket - Nyakurui	20. Janga Supermarket - Nyakurui	30. Mwangi Catholic Church - Nyakurui

M-PESA
Paybill number: 303030

LAIKIPIA COUNTY COVID-19 SUPPORT ACCOUNT
2154 5000 0000 0000 0000 0000 0000 0000 0000 0000
PAYBILL: 303230

FOR MORE INFORMATION CONTACT: 0716 031 031

Kusimamia Maisha ya Parokia wakati huu Zaka na Sadaka

Wakristu ambao wana uwezo wa kuendelea kusimamia kazi za Parokia kwa njia ya sadaka na zaka, au fungu la kumi (10%), wanaweza kuchangia wakati wowote hata kama hatuwezi kukutana kanisani.

- MICHANGO YA MAKANISA MADOGO** - Makanisa Madogo kadhaa yameshapanga jinsi ya kuchangia zaka au sadaka nyingine: viongozi wa Jumuiya Ndogo Ndogo wamepokea michango ya wanajumuiya, kisha kiongozi mmoja wa Kamati ya Kanisa ameleta bahasha zote katika Ofisi ya Parokia. Tuna-shukuru sana Wakristu walioweza kujitolea kusaidia Parokia hata wakati huu wa changamoto.
- MPESA** - Njia nyingine ni kutoa sadaka ama zaka kupitia huduma ya Mpesa, kwa namba ya Baba Paroko (0720169257 - Giacomo Basso), na kumwambia Padri mchango huo umetoka kwa nani na kwa sababu gani (kwa sms au kupiga simu).
- KANISANI OL MORAN** - Kanisa la Parokia ni wazi kwa ajili ya maombi ya Wakristu binafsi (bila mkusanyiko wa watu). Kunao walioacha sadaka zao katika sanduku iliyomo kanisani.

Kipindi cha Pasaka na Mwezi wa Bikira Maria

PASAKA - Jumapili ya Ufufuko, tarehe 12 Aprili, kilianza **Kipindi cha Pasaka**, kina-choendelea kwa muda wa siku hamsini, hadi sikukuu ya Pentekoste.

SHEREHE ZIFUATAZO - Sherehe ya Yesu **Kupaa Mbinguni** itakuwa Jumapili 24 Mei. Jumapili ifuatayo, 31 Mei, itakuwa Sherehe ya **Pentekoste**, siku ya Roho Mtakatifu

kushuka juu ya Mitume, mwanzo wa Kani-sa na wa kazi ya kueneza Injili. Ndipo mwisho wa kipindi cha Pasaka. Zitafuata Jumapili ya **Utatu Mtakatifu** (7 Juni), na Sherehe ya **Mwili na Damu ya Kristu** (14 Juni).

MWEZI WA MARIA - Mei ni **mwezi wa Bikira Maria**, tunayemheshimu hasa kwa njia ya maombi ya Rozari Takatifu. Ingawa mwaka huu ni Pentekoste, tarehe 31 ni Sikukuu ya "Visitation" (Maria kumwambia Elizabeti), ndiyo sherehe ya Masista wetu.

COUNTING OF EASTER

Days of Easter Season are counted according to the timing of the Gospels and the Acts of the Apostles:

8 DAYS: From Easter Sunday to the Second Sunday, the Octave (= 8 days) is celebrated as one great festive day of the Resurrection of the Lord.

40 DAYS: From Easter to the Ascension, which is the period of the Apparitions of the Risen Lord to the Apostles.

50 DAYS: From Easter to Pentecost, i.e. the 50th day. It was the Jewish feast of the gift of the Law by God to Moses.

We now celebrate the gift of the Holy Spirit upon the Apostles, the new law of the Spirit. 50 is a number of perfection: 7 days (weeks) x 7 + 1, as a fullness of time.

Neno la Kanisa

Barua ya Papa Fransisko



Siku chache zilizopita, Baba Mtakatifu aliwaandikia Wakristu wote barua, akiwapatia moyo wa kusali nyumbani mwezi huu wa Bikira Maria, pia wakati wa janga la Coronavirus linalofanya familia nyingi zikae zaidi nyumbani.

Ni vema hata sisi tupate ujumbe wa Papa Fransisko, na tutumie katika familia sala hizi mbili tulizopewa naye.

LETTER OF HIS HOLINESS POPE FRANCIS TO THE FAITHFUL FOR THE MONTH OF MAY 2020

Dear Brothers and Sisters,

The month of May is approaching, a time when the People of God express with particular intensity their love and devotion for the Blessed Virgin Mary. It is traditional in this month to pray the Rosary at home within the family. **The restrictions of the pandemic have made us come to appreciate all the more this "family" aspect, also from a spiritual point of view.**

For this reason, I want to encourage everyone to rediscover the beauty of praying the Rosary at home in the month of May. This can be done either as a group or individually; you can decide according to your own situations, making the most of both opportunities. The key to doing this is always simplicity, and it is easy also on the internet to find good models of prayers to follow.

I am also providing two prayers to Our Lady that you can recite at the end of the Rosary, and that I myself will pray in the month of May, in spiritual union with all of you. I include them with this letter so that they are available to everyone.

Dear brothers and sisters, **contemplating the face of Christ with the heart of Mary our Mother will make us even more united as a spiritual family** and will help us overcome this time of trial. I keep all of you in my prayers, especially those suffering most greatly, and I ask you, please, to pray for me. I thank you, and with great affection I send you my blessing.

Given in Rome, 25 April 2020, Feast of Saint Mark the Evangelist
Pope Francis

FIRST PRAYER

O Mary, You shine continuously on our journey as a sign of salvation and hope. We entrust ourselves to you, Health of the Sick, who, at the foot of the cross, were united with Jesus' suffering, and persevered in your faith.

"Protectress of the Roman people", you know our needs, and we know that you will provide, so that, as at Cana in Galilee, joy and celebration may return after this time of trial.

Help us, Mother of Divine Love, to conform ourselves to the will of the Father and to do what Jesus tells us. For he took upon himself our suffering, and burdened himself with our sorrows to bring us, through the cross, to the joy of the Resurrection. Amen.

We fly to your protection, O Holy Mother of God; Do not despise our petitions in our necessities, but deliver us always from every danger, O Glorious and Blessed Virgin.

SECOND PRAYER

"We fly to your protection, O Holy Mother of God".

In the present tragic situation, when the whole world is prey to suffering and anxiety, we fly to you, Mother of God and our Mother, and seek refuge under your protection.

Virgin Mary, turn your merciful eyes towards us amid this coronavirus pandemic. Comfort those who are distraught and mourn their loved ones who have died, and at times are buried in a way that grieves them deeply. Be close to those who are concerned for their loved ones who are sick and who, in order to prevent the spread of the disease, cannot be close to them. Fill with hope those who are troubled by the uncertainty of the future and the consequences for the economy and employment.

Mother of God and our Mother, pray for us to God, the Father of mercies, that this great suffering may end and that hope and peace may dawn anew. Plead with your divine Son, as you did at Cana, so that the families of the sick and the victims be comforted, and their hearts be opened to confidence and trust.

Protect those doctors, nurses, health workers and volunteers who are on the frontline of this emergency, and are risking their lives to save others. Support their heroic effort and grant them strength, generosity and continued health.

Be close to those who assist the sick night and day, and to priests who, in their pastoral concern and fidelity to the Gospel, are trying to help and support everyone.

Blessed Virgin, illumine the minds of men and women engaged in scientific research, that they may find effective solutions to overcome this virus.

Support national leaders, that with wisdom, solicitude and generosity they may come to the aid of those lacking the basic necessities of life and may devise social and economic solutions inspired by farsightedness and solidarity.

Mary Most Holy, stir our consciences, so that the enormous funds invested in developing and stockpiling arms will instead be spent on promoting effective research on how to prevent similar tragedies from occurring in the future.

Beloved Mother, help us realize that we are all members of one great family and to recognize the bond that unites us, so that, in a spirit of fraternity and solidarity, we can help to alleviate countless situations of poverty and need. Make us strong in faith, persevering in service, constant in prayer.

Mary, Consolation of the afflicted, embrace all your children in distress and pray that God will stretch out his all-powerful hand and free us from this terrible pandemic, so that life can serenely resume its normal course. To you, who shine on our journey as a sign of salvation and hope, do we entrust ourselves, O Clement, O Loving, O Sweet Virgin Mary. Amen.

Njia tatu za Sala

Maombi Nyumbani

Hapa mnaweza kupata njia tatu za sala mnazoweza kutumia nyumbani wakati huu wa Pasaka na wa Mwezi wa Mei.

Maombi haya yaweza kufanywa pamoja na familia, ama kila mtu kivyake. Watoto pia wafunzwe kusali!

Tuwaombe watu wote, wagonjwa, wenye shida, marehemu.

Wanaohitaji Biblia au vitabu vingine vya sala, waweza kuvinunua katika Ofisi ya Parokia.

1- SALA YA KILA SIKU

Wakristu wakumbuke maombi ya kila siku, hasa asubuhi na jioni. Wasisahau ile sala ya saa sita (au saa nyingine ya mchana) kwa Mama wa Mfufuka, wakati wa Pasaka: Malkia wa Mbingu (badala ya sala Malaika wa Bwana).

MALKIA WA MBINGU (Kipindi cha Pasaka)

Malkia wa mbingu, furahi, aleluya.

- Kwani uliyestahili kumchukua, aleluya.

Ameufuka alivyosema, aleluya.

- Utuombe kwa Mungu, aleluya.

K. Furahi, shangilia, ee Bikira Maria, aleluya.

W. Kwani hakika Bwana amefufuka, aleluya.

Tuombe. Ee Mungu, uliyependa kuifurahisha dunia kwa kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristu Mwanao: fanyiza, twakuomba, kwa ajili ya Bikira Maria Mamaye, tupate nasi furaha za uzima wa milele. Kwa huyo Kristu Bwana wetu. Amina.

2- SALA YA ROZARI TAKATIFU

Sala ya Rozari ni maombi ambayo Wakristu hupenda sana popote duniani. Mwezi wa Mei ni Mwezi wa Maria, Wakristu hutumia sala hii kwa heshima ya pekee. Hapa mnakumbushwa utaratibu wa Rozari.

A) SALA ZA KUENZIA

Ishara ya Msalaba - Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.

Kumbuka - Kumbuka, ee Bikira Maria mpole sana, haijasikika hata mara moja kwamba ulimwacha mtu aliyekimbilia ulinzi wako, aliyeomba msaada wako na maombezi yako. Kwa tumaini hilo nakukimbilia wewe, Bikira wa mabikira, Mama yangu, naja kwako na kusimama mbele yako, nikilalamika mimi mkosefu. Ee Mama wa Neno wa Mungu, usikatae maneno yangu, bali kwa huruma yako upende kuyasikia na kuyasikiliza. Amina.

Kanuni ya Imani - Nasadiki kwa Mungu, Baba Mwenyezi, Mwumba mbingu na nchi. Na kwa Yesu Kristu, Mwanee wa pekee, Bwana wetu; aliyetungwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na Bikira Maria, akateswa kwa mamlaka ya Ponsio Pilato, akasulubiwa, akafa, akazikwa, akashukia kuzimu; siku ya tatu akafufuka katika wafu; akapaa mbinguni, amekaa kuume kwa Mungu Baba Mwenyezi. Toka huko atakuja kuwahukumu wazima na wafu. Nasadiki kwa Roho Mtakatifu, Kanisa takatifu katoliki, ushirika wa Watakatifu, maondoleo ya dhambi, ufufuko wa miili, na uzima wa milele. Amina.

B) MAFUMBO YA ROZARI

Kwa kila Fumbo:

- Kutangaza Fumbo (kufuatana na utaratibu wa kila siku).
- Kusali Baba yetu (x 1); Salamu Maria (x 10); Atukuzwe (x 1).

- Kisha, sala "Ee Yesu Wangu", pia wimbo unaofaa.

Ee Yesu wangu, utusamehe dhambi zetu, utuepushe na moto wa milele, ongoza roho za watu wote mbinguni, hasa za wale wanaohitaji zaidi ya huruma yako. Amina.

MAFUMBO YA FURAHA (Jumatatu na Jumamosi)

1. Malaika anampasha habari Maria kuwa Mama wa Yesu
2. Bikira Maria anakwenda kumtembelea Elisabeti
3. Yesu anazaliwa Bethlehemu
4. Yesu anatolewa hekaluni
5. Maria na Yosefu wanamkuta Yesu hekaluni

MAFUMBO YA MWANGA (Alhamisi)

1. Yesu anabatizwa katika mto Yordani
2. Yesu ageuza maji kuwa divai huko Kana
3. Yesu atangaza Ufalme wa Mungu
4. Kugeuka sura kwa Yesu
5. Kuwekwa kwa Ekaristi



MAFUMBO YA UCHUNGU (Jumanne na Ijumaa)

1. Yesu anasali katika bustani Gethsemane
2. Yesu anapigwa mijeledi
3. Yesu anatiwa taji la miiba
4. Yesu anaubeba msalaba wake
5. Yesu anakufa msalabani

MAFUMBO YA UTUKUFU (Jumatano na Jumapili)

1. Yesu amefufuka
2. Yesu anapaa mbinguni
3. Roho Mtakatifu anawashukia Mitume siku ya Pentekoste
4. Maria anapalizwa mbinguni
5. Maria anavikwa taji kuwa Malkia

SALA ZA KUMALIZIA

Salamu Malkia - Salamu, Malkia, Mama mwenye huruma; uzima, tulizo na matumaini yetu, salamu. Tunakusihia ugenini hapa, sisi wana wa Eva. Tunakulilia, tukilalamika na kuhuzunika bondeni huku kwenye machozi. Haya, basi, Mwombezi wetu, utuanguale kwa macho yako yenye huruma. Na mwisho wa ugeni huu, utuonyeshe Yesu, mzao mbarikiwa wa tumbo lako. Ee mpole, ee mwema, ee mpendevu, Bikira Maria.

(Litania ya Bikira Maria huweza kuongezwa, na Wimbo wa kumalizia. Pia, Sala ya Papa Fransisko: tazama uk. 2)

3- MASOMO YA KILA JUMAPILI

Siku ya Jumapili, Wakristu afadhali watafakari Neno la Mungu katika masomo haya ya Injili na Biblia ya kila Jumapili ya Mei.

Walio na Biblia nyumbani, waweza kutumia hata sala ya Zaburi zilizotajwa hapa chini. Pia, waweza kutazama katika Kalenda (au Diary) marejeo ya masomo ya kila siku.

3 Mei — JUMAPILI YA 4 YA PASAKA

Mchungaji na Mlango wa Uzima

Jumapili ya Mchungaji Mwema, Jumapili ya Miito

✧ Injili ya Yohane 10:1-10

Usiku wake wa mwisho, Yesu alisema "Kweli nawaambiini, yeyote yule asiyeingia katika zizi la kondoo kwa kupitia mlango, bali hupenya na kuingia kwa njia nyingine, huyo ni mwizi na mnyang'anyi. Lakini anayeingia kwa kupitia mlango, huyo ndiye mchungaji wa kondoo.



Mngoja mlango wa zizi humfungulia, na kondoo husikia sauti yake, naye huwaita kondoo wake kila mmoja kwa jina lake na kuwaongoza nje. Akisha watoa nje huwatangulia mbele nao kondoo humfuata, kwani wanajua sauti yake. Kondoo hao hawawezi kumfuata mgeni, bali watamkimbia kwa sababu hawajui sauti yake.”

Yesu aliwaambia mfano huo, lakini wao hawakuelewa alichotaka kuwaambia. Basi, akasema tena, “Kweli nawaambieni, mimi ni mlango wa kondoo. Wale wengine wote waliokuja kabla yangu ni wezi na wanyang’anyi, nao kondoo hawakuwasikiliza. Mimi ni mlango. Anayeingia kwa kupitia kwangu ataokolewa; ataingia na kutoka, na kupata malisho. Mwizi huja kwa shabaha ya kuiba, kuua na kuharibu. Mimi nimekuja mpate kuwa na uzima, uzima kamili.”

• **Zaburi 23 (Bwana ndiye mchungaji wangu)**

10 Mei — JUMAPILI YA 5 YA PASAKA
Yesu Njia, Ukweli na Uzima

✠ **Injili ya Yohane 14:1-12**

Usiku wa mwisho, Yesu aliwaambia mitume, “Msifadhaike mioyoni mwenu. Mwaminini Mungu, niaminini na mimi pia. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; la sivyo ningalikwisha waambieni. Sasa nakwenda kuwatayarishieni nafasi. Na nikienda na kuwatayarishieni nafasi, nitarudi na kuwachukueni kwangu, ili nanyi muwe pale nilipo mimi. Mnajua njia ya kwenda huko ninakokwenda.” Thomaso akamwuliza, “Bwana, hatujui unakokwenda, tutawezaje basi, kuijua hiyo njia?” Yesu akamjibu, “Mimi ndimi njia, na ukweli na uzima. Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu. Ikiwa mnanijua mimi mnamjua na Baba yangu pia. Na tangu sasa, mnamjua, tena mmekwisha mwona.”



Filipo akamwambia, “Bwana, tuonyeshe Baba, nasi tutatosheka.” Yesu akamwambia, “Filipo, nimekaa nanyi muda wote huu, nawe hujanjua? Aliyekwisha niona mimi amemwona Baba. Unawezaje basi, kusema: ‘Tuonyeshe Baba?’ Je, huamini kwamba mimi niko ndani ya Baba, naye Baba yuko ndani yangu? Maneno ninayowaambieni nyote siyasemi kwa mamlaka yangu; Baba aliye ndani yangu anafanya kazi yake. Mnapaswa kuniamini ninaposema kwamba mimi niko ndani ya Baba naye Baba yuko ndani yangu. Ama sivyo, aminini kwa sababu ya mambo ninayofanya. Kweli nawaambieni, anayeniamini atafanya mambo ninayofanya mimi; naam, atafanya hata makuu zaidi, maana nakwenda kwa Baba.”

• **Zaburi 33 (Mshangilieni Bwana, enyi wenye haki)**

17 Mei — JUMAPILI YA 6 YA PASAKA
Ahadi ya Roho aliye Msaidizi

✠ **Injili ya Yohane 14:15-21**

Usiku wa mwisho, Yesu aliwaambia mitume, “Mkinipenda mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba naye atawapeni Msaidizi mwingine, atakayekaa nanyi milele. Yeye ni Roho wa kweli. Ulimwengu hauwezi kumpokea kwa sababu hauwezi kumwona wala kumjua. Lakini ninyi mnamjua kwa sababu anabaki nanyi na yu ndani yenu.



Sitawaacha ninyi yatima; nitakuja tena kwenu. Bado kidogo nao ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mtaniona; na kwa kuwa mimi ni hai, nanyi pia mtakuwa hai. Siku ile itakapofika mtajua kwamba mimi niko ndani ya Baba, nanyi mko ndani yangu, nami ndani yenu. Azipokeaye amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye. Naye anipendaye mimi atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.”

• **Zaburi 66 (Mshangilieni Mungu kwa furaha)**

24 Mei — JUMAPILI YA BWANA KUPAA MBINGUNI
Enendeni, mkawafunze mataifa

KUMBUKUMBU

Yesu alipaa Mbinguni - Baada ya Ufufuko, Yesu alijionyesha mzima kwa Mitume. Baada ya muda wa siku arobaini, akapaa mbinguni, akaketi kuume kwa Mungu Baba.

Amri ya Kuhubiri Injili - Kabla ya kuagana na Mitume, aliwaamuru kuhubiri Injili yake duniani kote, akawaahidia msaada wa Roho Mtakatifu.

✠ **Injili ya Mathayo 28:16-20**

Baada ya ufufuko wa Yesu, wale wanafunzi kumi na mmoja walikwenda Galilaya kwenye ule mlima aliwaagiza Yesu. Walipomwona, wakamwabudu, ingawa wengine walikuwa na masha-ka. Yesu akaja karibu, akawaambia, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati.”



• **Zaburi 42 (Enyi watu wote, pigeni makofi)**

31 Mei — JUMAPILI YA PENTEKOSTE
Wote walijaa Roho Mtakatifu

KUMBUKUMBU

Roho Mtakatifu ashuka juu ya Mitume - Kabla ya Mateso, Yesu aliwaahidia Mitume Roho Mfariji wa Mungu. Jumapili ya Ufufuko, Yesu aliwasalimu Mitume: “Amani iwe kwenu”, akawavuvia, akawashushia Roho Mtakatifu. Kisha, siku ya Pentekoste, yaani Siku ya Hamsini baada ya Ufufuko, Roho wa Mungu alishuka juu ya Mitume.

Mwanzo wa Kanisa - Leo tunasherehekea pia siku ya kuzaliwa kwa Kanisa la Yesu moja, takatifu, katoliki, la kitume, wakati Mitume walipompokea Roho na kuanza kuhubiri.

Vipaji Saba vya Roho (taz. Is 11:2) - 1. Hekima - 2. Akili - 3. Shauri - 4. Nguvu - 5. Elimu - 6. Ibada - 7. Uchaji wa Mungu.

✠ **Matendo ya Mitume 2:1-11**

Siku ya Pentekoste ilipofika, waumini wote walikuwa wamekusanyika pamoja. Ghafla, sauti ikasikika kutoka angani; sauti iliyokuwa kama ya upepo mkali, ikajaza ile nyumba yote walimokuwa wamekaa. Kisha, vikatokea vitu vilivyoonekana kama ndimi za moto, vikagawanyika na kutua juu ya kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema lugha mbalimbali kadiri Roho alivyowawezesha.



Na huko Yerusalemu walikuwako Wayahudi, watu wamchao Mungu, waliotoka katika kila nchi duniani. Waliposikia sauti hiyo, kundi kubwa la watu lilikusanyika. Wote walishtuka sana kwani kila mmoja wao aliwasikia hao waumini wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Walistaajabu na kushangaa, wakisema, “Je, hawa wote tunaowasikia wakisema hivi, si wenyeji wa Galilaya? Imekuwaje, basi, kwamba kila mmoja wetu anawasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe? Baadhi yetu ni Waparthi, Wamedini na Waelami; wengine ni wenyeji wa Mesopotamia, Yudea, Kapadokia, Ponto na Asia, Frugia na Pamfulia, Misri na sehemu za Libya karibu na Kurene; wengine wetu ni wageni kutoka Roma, Wayahudi na watu walioongokea dini ya Kiyahudi; wengine wametoka Krete na Arabia. Sisi sote tunasikia wakisema kwa lugha zetu wenyewe mambo makuu ya Mungu.”

• **Zaburi 104 (Umsifu Bwana, ee roho yangu)**

SAUTI ya Mtakatifu MARKO

- No. 80, Year 12, Printed on 30th April 2020 - (NOT FOR SALE)

SAINT MARK CATHOLIC PARISH - Ol Moran - Catholic Diocese of Nyahururu
P.O.Box 20 - 20320 Kinamba - saintmark@olmoran.it - +254 720 924 153